
# Shule Ya Biblia Ulimwenguni Kwa Njia Ya Kideo

**Ilianza 1986**



# ELIMU YA KUTUNGA NA KUTOA HOTUBA

**HOMILETIKSI**

*Mafunzo haya yametengenezwa ili ya saidie wanafunzi Shule ya Ulimwengu kwa njia ya ya kideo wasiotafuta kutunukiwa, wanaosomea nyumbani kwa kupata cheti. Mwanafunzi atatakiwa kuweka bidii katika mtaala mzima. Mwanafunzi asiyetaka kutunukiwa anaweza asijali kufuata mtaala na kutumia mafunzi apendavyo kwa manufaa yake ya kiroho.*




Shule  Ya Biblia Ulimwenguni Kwa Njia Ya Kideo
130 Lantana Lane
Maxwell, Texas 78656-4231
Marekani.

*biblestudy@wvbs.org*
*http://www.wvbs.org/*

Shule Ya Biblia Ya Arusha
Sanduku la Barua 12163 Arusha
Tanzania.

YALIYOMO

Mtaala……………………………………………………………………………….Ukurasa 1

Mafunzo…………………………………………………………………………………4

Nyongeza……………………………………………………………………………….58

**MTAALA**

**HOMILETIKSI**
**(ELIMU YA KUTUNGA NA KUTOA HOTUBA)**

**I. HABARI KWA UJUMLA**.

A. Mkufunzi: Francis Wechesa.
B. Kozi hii inayo masomo 23
C. Kila darasa linachukuwa takribani dakika 45

II. **MAELEZO NA KUSUDI**.

A. Hii ndiyo kujifunza Homiletiksi, sanaa ya kutunga na kutoa hotuba.
B. Tutalia mkazo utendaji
C. Wanafunzi atajifunza kutayarisha muhtasari wa mawazo ili aweze kuyatoa katika maneno.
D. Wanafunzi watajifunza kuchanganua, kubiliana uoga wakati wa kutoa somo, kusolewa, na kuwa tayari kumzungumza Bwana ipasavyo.

**II. VIFAA VYA MAFUNZO**.

A. Yatakayotakiwa:
   1. Biblia
   2. Kanda za Kideo
   3. Karatasi za kozi

**III. YATAKIWAYO:**

A. Tazama kanda
B. Soma notisi za darasani
C. Fanya madondoa yote.
D. Kila mwanafunzi atatakiwa kuunda na kutoa hotuba.
E. Kutakuwa na mitihani miwili.

   1. Kati ya muhula
   2. Mwisho wa muhula

F. Mistari ya kudondoa:
Mdo. 8:4
Warumi 1:16
Rumi.10:14
1Korintho 1:21
1Korintho 9:16
Galatia 1:8
2Tim. 4:1-5

## MAMBO YA UTANGULIZI

**I. Kusudi ya Kozi hii:**

A. Kuwapa uhakika wale wanaotamani kuhubiri.
B. Kutoa habari namna unavyoweza kuchagua, kutayarisha, na kuwapa watu maneno kutoka kwa Mungu ili iwe na matokeo ya kuwabadilisha maisha wasikilizaji wako.
C. Kuonyesha hitaji na umuhimu wa kuhubiri neno la Mungu kwa Wakristo na wasio Wakristo. Kuwatunza waliookoka wabaki wameokoka na kuokoa waliopotea.

**II. Fafanusi:**

A. **HOMILETIKSI**:-Sanaa ya kutunga na kutoa hotuba
**HOTUBA**:- Namna ya kuwaelezea watu ukweli wa dini unaopatikana katika maandiko matakatifu, wenye kushawishi.

**III. Ni lini hotuba huonekana kuwa imefaulu?**

A. Ikiwa inakubaliana na neno la Mungu.- 2Tim. 4:2;1Pt.4:11
B. Ikiwa imehubiriwa katika upendo.- Efeso 4:15;2Tim.4:2
C. Ikiwa imetayarishwa kukidhi mahitaji ya wasikilizaji- Mathayo 4:4; Yohana 4:4-42
D. Ikiwa imezungumziwa kiasi kwamba wote wameelewa.- Marko 12:37; 1Korintho 14:19
E. Ikiwa inamtukuza Mungu.

**IV. Umuhimu wa Kozi hii:**

A. Watu hawapendi kusikiliza hotuba; kwa hiyo hata tukizungumza neno la Mungu tuna uhakika kwamba watatusikiliza.
   1. Kwa hiyo tunahitaji kujifunza kupata usikivu wa watu.
      a. Ilionekana watu walimsikiliza Yesu kwa makini.
      b. Siku hizi kuna upizani mwingi sana.
   2. Taratibu tofauti zimekuzwa katika miaka mingi itakayokusaidia kushika usikifu wa watu. Tutajifunza utaratibu huu katika darasa hili.

B. Unahitaji pia kuasilisha neno la Bwana ili watu wapate kuokolewa.
   1. Mahubiri mengi siku hizi hayalengi kuokoa roho za watu.
   2. Mahubiri mengi siku hizi yanayolenga kuokoa roho za watu hayaeleweki na kufahamika na wasikilizaji.
   3. Mashitaka mengi siku hizi kuhusu hotuba:
      a. Hotuba nyingi huchosha wasikilizaji.
      b. Somo halihusiani na mahitaji ya wakati huo ya wasikilizaji.
      c. Mahubiri hayana uhodari.
      d. Mahubiri hayaasilishi ujumbe.
      e. Mahubiri hayalengi kubadilisha maisha ya wasikilizaji.
      f. Mahubiri yenyewe yamewekewa mkazo zaidi.

**V. Kanuni usiyoweza kuvunja katika mazungumzo ni kuasilisha kwa kuleta lililotakiwa.**

A. Tunachukulia kwamba mwanafunzi anakubaliana kwamba neno la Mungu pekee ndilo linalotakiwa kuhubiriwa. Kwa hiyo, kozi inalenga kukusaidia kufahamu namna ya kutumia neno la Mungu.
B. Kanuni katika homiletiksi ni mazoea yale ambayo yameonekana kuwa yenye mafanikio kwa watu wengi. Kwa hiyo tukisema, “kanuni ya pekee

usiyoweza kuvunja ni kuasilisha kwa kuleta mafanikio" tunazungumzia kuhusu kanuni zile ambazo zimeonekana kuwa na mafanikio zaidi hazikufai wewe mahali uliko.

1. Kwa mfano tamaduni tofauti, umri (wazee dhidi ya vijana)
2. Walakini usije ukadhania kwamba kanuni na miongozo tutakazo toa hazitakufaa kabisa kwa sababu hazifanani na zile ulizozizoea. NYINGI YA KANUNI HIZI NI ZA WOTE.

VI. Mahitaji kadhaa kwa mahubiri au mafundisho yenye mafanikio:

A. Kuwa mtu wa kiroho.
   1. Ralph W. Emerson alisema, "Siwezi kusikia unachokisema kwa sababu ya jinsi ulivyo inavuma zaidi masikioni mwangu."
   2. Pamoja na kuwa kwamba kozi hii haijaundwa kumfanya mwanafunzi kukomaa kiroho, lakini inafahamika kwamba kila mmoja anayetamani kuhubiri ama kufundisha neno la Mungu, atafanya bidii kuwa kama Yesu kabla na wakati anapochukuwa wajibu mkubwa huo. (Tazama Yakobo 3:1).

B. Vipawa vya asili.
   1. Fikira safi.
   2. Kujisikia kupenda kuhubiri.
   3. Kuwa na nguvu za ubunifu katika kuwaza.
   4. Kuwa na uwezo wa kuongea
   5. Kuwa na afya nzuri.
   6. Kuwa na hamu ya kuasilisha.

C. Maarifa.
   1. Kuhusu ukweli wa Mungu wa milele.
   2. Kuhusu asili ya mwanadamu
   3. Kuhusu ulimwengu unaowazunguka.

D. Ujuzi.
   1. Katika mtindo.
   2. Katika kukusanya, kuchagua, na kupanga vitu.
   3. Katika kufikiria kimaantiki.

VII. Hatari ya kujifunza Homiletiksi.

A. Inavyozidi kuwa zuri, ni rahisi kuishia kutafuta sifa.
   1. Mdo. 12:22,23- Herode.
   2. Kwa kuwa wengi wameharibu mimbari kwa sababu hii, haina maana kwamba tuache kujifunza homiletiksi.
   3. Kutiwa moyo ni kuzuri, wengi wasingeendelea kuhubiri kama hakuna wanaowatia moyo.

B. Mkazo zaidi kuhusu kanuni na taratibu.
   1. Ni rahisi kufikiria kuhusu vitu ambavyo umejifunza katika homiletikisi badala ya kufikiria kuhusu kile unajaribu kuasilisha.
   2. Kuwa msemaji sio jambo la msingi, bali "kutoa ukweli unaoandama na tabia nzuri katika maisha ya mtoa ujumbe."
   3. Kanuni haziko juu ya utaratibu(tabia za asili) (usiwe mtumwa wa kanuni za homiletiksi).

C. Inaweza kukuzuia usisikilize kanisani kwa kuwa makini kutafuta makosa katika mtoa hotuba.(namna anavyotoa)

D. Inaweza kukufanya usimtegemee Mungu na baraka zake kwa sababu hutokea haraka kutunga na kutoa hotuba.

E. Mwigo.
   1. Aina mbili- Ya kufahamu moyoni na yakutofahamu moyoni
   2. Tunaweza kutengena nayo kwa kujichunguza nafsini mwetu. (tumia kada ya redio ama ya kideo kujikosoa.
   3. Tatizo kubwa ni kuiga makosa ya mtu mwingine.
      a. Ni makosa yale ambayo ni dhahiri. "Ni sanaa ya hali ya juu kuficha sanaa."
      b. Unapojaribu kuiga watu ambao wamefaulu ili ujifunze siri ya mafanikio yao, utajifunza kwamba siri yao kuu ilikuwa kwamba, hawakuhitaji kuiga mtu yeyote.
      c. Unaweza kujikuta anajaribu kuiga mtu ambaye anajitahidi kushinda makosa yake.

VIII. Malengo ya kozi hii.

A. Kujifunza maarifa ya kutunga hotuba.
B. Kukuza mantiki ya wazi ya hotuba za kimaandiko.
C. Kutafuta njia ya kukufanikisha wewe na mtindo wako.
D. Kuzoea kuwa mbele ya wasikilizaji.

## HOFU YA JUKWANI

**I. Hili ni tatizo la kawaida kwa kila anayeanza kuzungumza.**

**II. Visabibishaji hofu:**

A. Kukosa kujitayarisha vya kutosha.
B. Hali yakujifikiri mwenyewe.
   1. Kuogoba kushindwa
   2. Kuogopa kukosea
   3. Kuogapa kwamba utachekwa

C. Kuhofia wasikilizaji
   1. Ni jambo la kawaida kuwa sehemu ya kundi lakini sio kuwa mbele yao. Katika mazungumzo, ukinyamaza, mtu mwingine anaweza kusaidia. Pia ukitaka kunyamaza unaweza. Hapa itategemea wewe mwenyewe.
   2. Uajibu usio wa kawaida wa kuhubiri ule ambao utaamua mwisho wa milele wa mtu.

**D.** Kutojua

III. **Dalili za hofu za jukwani**

A. Unakuwa na uoga kutoka ndani; na baadaye inatoka nje, n.k. inatoka ndani akili ikipingana na chochote unachogusa kinaweza kukutisha.
B. Kushindwa kuwatazama wasikilizaji wako.
C. Unakuwa na matatizo katika kumeza
D. Unaanza kutetemesha.
E. Moyo unadunda
F. Unakuwa na shida katika kupumua
G. Mdomo unakuwa mkavu
H. Unakuwa na jasho la ziada
I. Unasahau

J. Unashindwa kutingishika au unatingishika sana.
K. Unakosa ujasiri
L. Kuwa na gugumizi.
M. Unakuwa na shida katika sauti.

**IV. Msaada katika kuondoa hofu ya jukwani.**

A. Omba.
B. Kuwa na hamu ya kuasilisha ujumbe wako.
C. Jaa na shauku kuhusu mazungumzo yako.
D. Chagua somo linalokupendeza unalolifahamu tosha.
E. Fahamu somo lako vema, jitayarishe katika sehemu zote; usilikariri neno kwa neno, kuwa na maandishi mazuri.
F. Lenga kuasilisha ujumbe wako kwa wasikilizaji wako
    1. Wanachokihitaji watu ni ujumbe.
    2. Akili na moyo wako uwe juu ya ujumbe wako.
    3. Tambua mahitaji ya wasikilizaji wako.
G. Vaa vizuri na uwe msafi.
H. Usijaribu kuwavutia wasikilizaji wako kwa kutumia maneno magumu, kuonyesha uhodari wako katika maarifa yako.
I. Jiaamini.
J. Zungumzo kila upatapo nafasi.
K. Ondoa wasiwasi kwa kutumia vitendo vifuatayo:
    1. Piga miayo, chezesha mikono na miguu, vuta pumzi.
    2. Tumia mwili katika utoaji ili kuachilia nguvu.

V. **Thamani ya uhofu ya jukwani.**

A. Inakupa nguvu unazoweza kuzielekeza katika nguvu, na maandalizi ya kuwa na shauku.
B. Inakufanya uwe na tamaa ya kujiandaa vya kutosha.
C. Inakusaidia kukumbuka kuwa mpole.

## MCHANGUNUO WA WASIKILIZAJI

I. **Kusudi na maana.**

A. Inaamua ni nini utakacho wafundisha au hubiria wasikilizaji wako.
B. Inaamua ni mjio gani utakayotumia kuhusu somo lako kwa wasikilizaji wako.

**II. Sehemu mbili kuu katika mchanganua wa wasikilizaji.**

A. Sehemu za kuamua ni nini cha kuhubiri(fahirisi)
    1. Ufahamu wa Biblia ulionao.
    2. Dhambi dhahiri
    3. Ushirikiano wa wandugu.
    4. Hudhurio
    5. Nia au tabia
    6. Kiasi gani ya kazi ya kikristo unayoifanya ukiwa mbali na jingo la kanisa.
    7. Tabia katika ibada na katika madara
        a. Je, wanaleta Biblia
        b. Wanafika mapema au wanachelewa
        c. Je, wanazungumza wakati wa ibada.
        d. Wanakaa wima, karibu, wakiwa wamelala nyuma?
    8. Watu wanje wanawasemaje.
    9. Vitu unavyovigundua unapowatembelea manyumbani mwao.
        a. Hali ya nyumba yao.
        b. Mazungumzo ya familia yao.
    10. Mavazi yao(Baba, mama, watoto) Watu wanayo mazoea ya kuvaa wapendavyo.

III. **MUDA WA HALI YA WASIKILIZAJI**.

A. Kabla ya kuanza mahubiri au kufundisha darasa.
B. Ukiwa mbele—Tazama vitendo vya wasikilizaji wako, daima watangulie, wafanye wakusikilize na kukufahamu.

NAMNA YA KUANDAA SOMO LAKO KUFUATANA HALI YA WASIKILIZAJI

I. Mapokezi- Ya kirafiki.
  A. Kuwa mfano halisi, mwenye nguvu, tayari daima.
  B. Ubishi mwingi hautakiwi.
  C. Amusha,himiza, na kutia hamu.
II. Ya kutojali-kuwapo lakini anajali kidogo.
  A. Onyesha kwa nini ni muhimu.
  B. Kama mpya, hakikisha wanafahamu.
  C. Tumia mambo hasa, matukio waliyowahi kutokea, toa malinganisho, mifano.
  D. Wajaze na uaminifu, bidii, utendaji, na uthabiti wako mwenyewe.
III. Wenye wasi wasi(Mashaka)- “Nitasikiliza, lakini nina wasi wasi.”

  A. Kuwa mtoa taarifa (wakati mwingine ukosefu wa taarifa huleta wasi wasi.
  B. Usiwalemee na manukuu ya zamani, yasiojulikana sana.
  C. Panga maendeleo vema.
  D. Fafanua sahihi- Kosa moja litaweza kuharibu hotuba yako zima.
  E. Onyesha namna mambo hayo yanavyohusiana na maisha yao.
  F. Tumia mifano, malinganisho,
IV. WANAOPINGA.

  A. Fahamu wasikilizaji wako wanachokikubali kama ukweli (Haitasaidia kuwanukulia vifungu vya Biblia kama hawaamini kwamba biblia ni neno la Mungu.
  B. Tumia ukweli, kuwa na uhakika nao.
  C. Anza na ukweli unaokubalika ili wasije wakasema, “sikuamini.”
  D. Wafanye wakuamini na kukupenda na kukubali uwezo na uaminifu wako.
  E. Kuwa mzuri, usipindishe msimamo makosa na kuufanya kuonekana wa ajabu(unaweza kuwafanya wasikilizaji wako kuanza kujitetea) au kuwafanya kuwa dhaifu hata kuliko walivyokuwa.
    1. Wakigundua tofauti hoja zako zote zitaharibika.
    2. Ni kuonyesha kutokuwa mwaminifu
  F. Elewa mahitaji ya kimsingi ya wasikilizaji wako (Ikiwa wanataka kuamini kugeuka ili wawe kama wanyama, ukibishana nao hutafikia kwa kutumia ukanusho wa kugeuka(evolution) hutafikia lengo lako
  G. Wape kitu bora kuliko kile walicho nacho,lakini kwanza wafanye watambue walicho nacho.
  H. Tafuta ni nini kilichowafanya kuamini walichotangulia kuamini na kukishinda hicho,(kwa mfano baba na mama waliamini hivyo na walikufa kwa hiyo siwezi kubadilika)

**WAZO KUU(WK)**

I. MANENO YENYE MAANA ILE ILE(SYNONYMS) Kisa , wazo la wazi, kusudi, shabaha, insha, na hoja
II. FAFANUSI: Katika kila hotuba lazima kuwa na wazo moja lenye kuongoza utaratibu mzima na kusudi la somo.

III. TOFAUTI KATI YA SOMO NA JINA, WK.

A. Somo(au Kiini cha habari)- Ni aina itakayo husika katika kila msitari wa Biblia kuhusiana na somo husika.

B. Jina la heshima- Hili linakusudia kuteka akili za wasikilizaji na kuwapa hamu Halihusiki na utaratibu wa hotuba.

C. W.K.- Hili hujibu swali, kwa nini alihubiri hotuba hii?

IV. UMUHIMU WA W.K.(INSHA)

A. Ina hakikisha umoja katika hutuba, na umoja huo huhakikisha yafuatayo:
   1. Mafundisho
   2. Thibitisho la hatia ya kosa
   3. Ushawishi wa kubadilisha tabia

B. Inasaidia huondoa mambo ambayo hayafai katika ujumbe moja.

V. MANUFAA YA W.K.(INSHA) No. 20

A. Humlazimisha msemaji kufikiria kupitia somo lake na kufikia lengo Fulani.

B. Humlazimisha msemaji kufinya somo lake kuwa lile linaloweza kuwezekana katika hotuba moja kwa kipimo cha muda alionao.

VI. SIFA ZA W.K.(INSHA)

A. Ndiyo maana hasa ya hotuba (Itakuwa sawa na ile unayohatimisha nayo) Ndilo kusudi la kuhubiri hotuba hiyo.

B. Hutofautiana kufuatana na kusudi:
   1. Wakati mwingine ni inisha inayodai mantiki katika kuitbibitisha.
   2. Wakati mwingine ni ukweli unaokubalika unaohitaji kufafanuliwa.
   3. Wakati mwingine halitajwi mapema ikiwa ni kwa kusudi la kuwa “shitua” wasikilizaji.

VII. MAPENDEKEZO KUHUSU W.K.(INSHA)

A. Elezea W.K. lako wazi na dhahiri.

B. Andika W.K. na uwe nalo mbele yako wakati wote wa kutayarisha somo lako.

C. Usiandike kwa ufupi sana,

D. Pambanisha W.K.(Inisha) yako, na mchanganuo wa wasikilizaji wako.

E. Hakikisha wasikilizaji wako wanaelewa W.K. lako,(vingine nevyo hawataelewa kwa nini umehubiri.) No.21

*F. Fungamanisha pointi zako kuu na W.K.(Inisha) yako*

G. Unganisha itiko inayotakikana na W.K. (insha) yako, vinginevyo wasikilizaji wako hawatajua ni nini cha kuitikia.

H. W.K. karibu huwa inarudiwa daima katika hitimisho.

I. Sahihisha W.K. ikihitajika.
   1. Kwa kuanza, chagua W.K. la kujaribia.
   2. Baada ya kujifunza na kutafiti unaweza kutaka, au kuhitaji kusahihisha W.K.
      a. Unaweza ukajikuta kwamba maandiko matakatifu hayaungi mkono W.K. yako ya kujaribia.
      b. Kunawazekana kuhitajika badiliko kufuatana na wasikilizaji wakusudiwa kuanzia wakati wako wa kuanza kutunga hotuba yako hadi kufikia wakati wako wa kuitoa.
      c. Inaweza isitimize lengo lako ulilolikusudia (hotuba kuhusu kucheza, kwa hiyo anza kutafuta maandiko yanayokataza karama za ulevi na ulafi, ukware, n.k. lakini amua kuhubiri kuhusu kufanyika mtakatifu, n.k.)
   2. Ukisha maliza, cheki utaratibu wako na W.K. mpya, pia cheki na W.K. na mchanganuo wa wasikilizaji wako mpya.

IX. NAMNA YA KUCHAGUA NA KUAMUA W.K. YAKO:

A. Mchanganuo wa wasikilizaji- Mahitaji yao.

B. Kusoma pa pana sana,(ingawa unaweza kuona hitaji, unaweza usifahamu namna ya kutengeneza somo la kusuluhisha hadi utakaposoma zaidi na kugundua mjio mpya, ubishi mpya, maandiko matakatifu usioyafahamu.)
C. Andaa masomo kadhaa kwa wakati mmoja.
D. Ukiwa lengo la muda mrefu litakusaidia kuamua ili kusudi kufikia lengo lako.
E. Amua W.K. ukilitoa kwenye fungu la maandiko au somo.

1. Elezea dhana pana na kuacha sehemu zenyewe kujitokeza kama W.K. (kwa mfano,- Toba: Kwa nini? Nani? N.k.)
2. Tumia neno lionyeshao uhusiano uliopo kati ya kiumbe kingine a u kitu kingine (preposition), kiungo, namna ya kiarifa inayotumika kama neno liongezalo maana ya jina ili kuonyesha uhusiano kati ya masomo ili kupata W.K. moja. (kwa mfano. Wokovu kwa neema: Watoto nyumbani, n.k.)

X. MIFANO YA W.K.
A. 1Tim. 4:12 (Mfano kama Mhubiri kijana ndiyo W.K.)
B. Yakobo 1:19,20 (Nia sahihi kuhusu neno la Mungu)
C.Danieli 1:1-20 (Kufanya kilicho sahihi katika Bwana wakati shinikizo la kufanya makosa linaweza likakuzawadi.)

W.K. linapaswa kuwasaidia ujinga wa wasikilizaji kuhusiana na somo

**MANENO MACHACHE (AUTILAINI AU UMBO LA HOTUBA)** No.22

Ubora wa hotuba utategemea ubora wa autiline

**UTANGULIZI**

A. Mjenzi wa nyumba hutengeneza ramani na kisha kuifuata.
B. Kadhalika mhubiri anapaswa kutayarisha autilaini katika kuandaa na kutoa hotuba ili kuwa na mafanikio.
C. Autilaini ina matumizi na yatakiwayo Fulani.

MWILI

I. Matumizi ya autilaini No. 23
A. Autilaini inapaswa kufanya kama mwongozo katika ujenzi wa hotuba. (Nimtumishi sio mtawala)
1. Inasaidia kuchagua vitu vyakufanyia kazi.
2. Inasaidia katika kupanga vitu vyakazi ulivyo vichagua.
a. Kwa kusadia mantiki
b. Kwa kusaidia kuwa na utaratibu zaidi.
c. Kwa kukusaidia kuwa mshawishi zaidi.
d. Kwa kusaidia kufanya somo kuhusishwa katika maisha ya wasikilizaji.

No.23 B. Autilaini inapaswa kutumika kama mwongozo katika utoaji wa somo.
1. Inamsaidia mhubiri katika kuwa na uthabiti katika utoaji.
2. Hutoa msingi wa notisi za msemaji kutazama anapozihitaji.
3. Inawasaidia wasikilizaji kufahamu na kuwa na usikivu.

II. Yatakiwayo ya autilaini.

A. Autilaini inapaswa kugawanywa katika sehemu tatu.

1. Utangulizi takribani d akika 10-15
2. Mwili muda mwingi wakutosha
3. Hatimisho takribani 5-10

B. Autilaini inapaswa kuonyesha uhusiano wa mawazo.

1. Tumia mpango wa kuacha pengo wakati wa kuanza msitari mpya.

2. Kwa kutumia alama zinazo faa.

a. I.

b. A.

c. 1.

d. a. No. 24

e. 1)

f. a)

g. B.

3. Kwa kutumia herufi kubwa, macho yetu yamezoea kusoma .

C. Autilaini yako inapaswa kubeba yote utakayohitaji kutoa katika hotuba.

1. Mawazo makuu yako yote
2. Mawazo ya kusaidia yote, yakiwa yametokuzwa vizuri.

D.Autilaini inapaswa kuwa fupi iwezekanavyo,lakini inayoeleweka.

1. Mawazo makuu yanatakiwa kuelezewa katika sentensi fupi.
   a. Lugha inayotumika yanapaswa kuwa sambamba na kila sehemu sambamba.
2. Mawazo ya kusaidia yanapaswa kuelezewa katika maneno muhimu, au fungu la maandiko.
3. Maandiko matakatifu rejea yasitumike kama vichwa vya pointi yako, bali vitumike kwa kuthibitisha au kutoa mwanga.

**HATIMISHO:**

A.Mtoa ujumbe anapaswa kuwa na uzoefu na kazi na hitaji la autilaini.

B.Mtoa ujumbe anapaswa kutayarisha autilaini kwa kila hotuba ili kutimiza kazi tulioelezea na kufuata kanuni zinazo zungumziwa.

C.Utayarishaji na utumiaji wa autilaini utaboresha uwezo wa mtoa ujumbe.

## AUTILAINI ITAKAYOHITAJIKA

ZINGATIA: Autilaini hii itahitajika darasani ili kukufundisha mambo ya msingi kadhaa lakini ni ujuzi unaohitajika kujenga hotuba. (Hotuba zote utakazo hotubia maishani mwako mwote sio lazima kufuata aina hii ya autilaini, ingawa autilaini hii sio kwa wale wanaoanza peke yao.

**Utangulizi**

A. Kupata usikivu

B. Wazo kuu.

   1. Lisitofautiane na fungu la maandiko ukiwa nalo.
   2. Unaweza kuamua kutoelezea wazo kuu kama kuna sababu ya kulifunuo katika hotuba yako inapoendelea.

C. Rudia kuangalia pointi zako kuu.

**MWILI**

I. Pointi kuu (ielezewi wazi wazi)

**A**. **THIBITISHA** kwamba pointi zako kuu ni sahihi na kweli.

1.Unaweza kutumia mfano kutoka Agano la kale.

2.Unaweza kunukuu maneno ya mtu anayetambulikana kuwa maarufu.
3.Inaweza kuwa maelezo ya mawazo.
4.Inaweza kuwa fafanusi ya mawazo.
5.Lakini kimsingi inatakiwa maandiko matakatifu kuthibitisha kwamba pointi uliyo elezea, ni kweli na yenye mafundisho ya kibiblia.

**B.MFANO(MLINGANISHO)**

1. Kusudi na aina itazungumziwa katika somo lingine.
2. Tumia mlinganisho ni muhimu sana( Yesu alitumia katika mafundisho yake)

**C.KUHUSISHA**

1. Hii nayo tutazungumzia katika somo lingine.
2. Hii ni muhimu sana, pia tunakosa katika jambo hili, kuwaelezea watu kinachofundishwa na biblia bila kuonyesha namna inavyowahusu, na nini wanachotakiwa kufanya.

**KUPITA KWENDA KATIKA POINTI NYINGINE**

ZINGATIA: KILA POINTI ITAFUATA AUTILAINI YA HAPO JUU(Pointi II,III, n,k.)
**HATIMISHO**

A.KURUDIA POINTI ZAKO KUU NI( KUONYESHA KWAMBA, UMEIMARISHA WAZO LAKO KUU – W.K.)

B. Fikisha wazo lako kuu panapotakiwa.
C. Tazamisha, yaani fanya wasikilizaji wako kuwa tayari kuitikia.

**KUSUDI LA HATIMISHO**

**I. Kusudi.**
A. Kutanisha hotuba yako nzima kwenye wazo lako kuu.
   1. Unganisha seheme zilizokuwa zikilegalega pamoja.
   2. Husisha mawazo yaliyokuwamo
B. Kuwashawishi wasikilizaji wako kutii.

**II. Mapendekezo kuhusu hatimisho:**
A. Fanya mwaliko kuwa sehemu ya hitimisho yako usitenganishe.
B. Fanya hitimisho kwanza(ikiwezekana hasa kimsingi)
C. Hakikisha hitimisho lako linafikisha kusudi lake, sio kupitia tu utaratibu.
D. Fanya wazo lako kuu akilini mwa wasikilizaji wako kufahamika.
E. Dumisha hali ya juu katika kuelezea kwako.
   1. Usitamke tu kile kinachokuja akilini mwako.
   2. Panga kila sehemu unayoifikia kama unavyoweza kupanga katika sehemu zingine za hotuba .
F. Usimalize kwa ghafla, hakikisha umefikia mwisho wako ulivyopanga.
G. Jitenge na mwisho usiofaa, kama, "somo letu limeishia hapo, muda wetu umekwisha, hayo ndiyo niliyokuwa nayo kwa leo."
H. Kuwa na mwisho wa uhakika moja, usitangetange, amua mahali pa kumalizia.
I. Usiwe mtu wa kuomba msamaha hasa kuhusiana na neno la Mungu.
J. Usipite kilele chako.
K. Usije ukaifanya ikaonekana kana kwamba haiwahusu.
   1. Kwa mfano: Msipotubu, msipokuwa katika kipimo, na sikitika kuwaambia kwamba, mko hatarini ya kwenda motoni na hali kama hiyo."
   2. Kwa hiyo husisha neno la Mungu moja kwa moja katika maisha yao.
L. Jitenge na mazoea ya kutumia mwaliko unaofanana mara kwa mara.

M. Usilete pointi mpya ile ambayo ingetakiwa kuwa katika mwili.
N. Jihadhari sana na kutisha, au kushindana, lakini elezea kinachotakiwa kufanywa kulingana na neno la Mungu.
O. Kuwa na wazo kuu la mwisho, na umalize vizuri.
P. Usiondoke,au kuacha autilaini yako haraka.
Q. Usionyeshe hasira, lakini wafanye wasikilizaji wako kupenda kuitikia.
R. Usiwe na hatimisho mrefu kuliko muda unaotakiwa.
S. Hatimisho yako iwe na usemi wako ule ule uliokuwa nao katika mwili wa hotuba.
T. Usitumie sentensi ndefu.

VI. Utaratibu unaotakiwa kufuatwa katika hatimisho:

A. Jumlisha kwa ufupi. Sema kwa maneno mafupi.
1. Kawaida—Elezea tena pointi kuu jinsi ilivyoelezewa.
2. Rudia pointi zako kuu, kwa kutumia lugha nyingine.
3. Kuwa mwerevu.—Weka kwa pamoja maneno mazuri yenye nguvu mtu anayoweza kukumbuka.
B. Nukuu:
C. Husisha wazo lako kuu.(W.K.)
1. Elezea namna maneno uliyoyatumia yanavyoweza kutumika.
2. Elezea namna kazi hiyo inavyoweza kutekelezwa.
3. Ingawa kila pointi inaweza ikawa na uhusiano yake yenyewe, Uhusiano huu, unaelezewa hadi ufahamike kwa kuwekea mkazo ili uwezekane kukumbukwa.
D. Elekeza:( Kwa mfano Mathayo 7:24 na kuendelea)
E. Tunga hadithi ya kuelezea mbele ya watu.
F. Pendekeza hatua kwa hatua za utendaji.
1. Hii inaweza kuwa pointi katika hotuba.
2. Wahubiri wengi husema fanya lakini hawaelezei namna ya kufanya.
G. Rudia utaratibu uliotumika katika utangulizi.
H. Wape changamoto.
I. Kusudi binafsi ( Unaweza ukasema, Wazee, na mashemasi wanatoa 10% na zaidi, je na wewe ungependa kutoa hivyo?)
J. Pointi ihusuyo tabia ya nchi (hali ya hewa)
1. Pointi zikiwa ndizo zinazojenga msingi, na hatimisho yako inapaswa kutokana nazo, unaweza ukafanya pointi yako ya mwisho kuwa ya kwanza.
2. Mfano wa hotuba wa Lloyd Deal.
VII. UKWELI UNAOKOA- UBATIZO
VI. KUBALI UKWELI
V. KUWA KIU YA UKWELI
IV. KUJIHADHARI NA WALIMU WA UONGO
III. WOKOVU NI KATIKA KRISTO
II. BIBLIA NDIYO YENYE MAMLAKA HAYO
I. MAMLAKA YA KRISTO.
K. Maneno katika wimbo, hasa wimbo wa mwaliko.
L. Shairi
M. Sala (lakini sio kama “ala”)

IV. UMUHIMU WA HATIMISHO.
A. Hotuba zima huubiriwa ili kupata hatimisho.
B. FANYA KAZI JUU YA HATIMISHO ILI ZIWE ZENYE NGUVU, ZA LAZIMA, NA ZA MUHIMU KWA HOTUBA. Si vigumu kufanya hili kwa wangalifu ikiwa kwa uhakika unahubiri kutokana na mahitaji yao na kutaka waende mbinguni.

## MAMBO YA MSINGI YA HOTUBA

I. Je, "fungu la maandiko" litumike( km. Ni lazima hotuba kutegemea fungu la maandiko fulani litakalo somwa mwanzoni?)

A. Faida za hotuba kutegemea fungu la maandiko:

1. Inakuwezesha kuzungumza kwa ujasiri kuhusu somo lako na hutoa mamlaka kwa kichwa cha somo lako.

ZINGATIA: Inaonekana siku hizi, hotuba zilizo nyingi hazitegemei fungu la maandiko. Hili ni jambo la kusikitisha.

2. Vifungu vingine vya maandiko hutumika kama msaada wa kumshutusha mtu ili kuelewa somo analokwenda kujifunza.
3. Linamsaidia msikilizaji kukumbuka kile anachofundishwa (hasa akiwa na mazoea na fungu hilo)
4. Muda wa kusoma fungu la maandiko utamfanya msikilizaji kukumbuka mawazo aliyokuwa nayo kuhusu fungu hilo. Linasaidia kutunza kumbukumbu akilini.
5. Linatusaidia kutoondoka katika mafundisho ya **Kiblia na kutufanya kubakia katika Biblia.**
6. Linatupatia uchaguzi. Fungu la maandiko linatusaidia mwongozo na mazingira.

B. Wakati ambao nisingelipenda kutumia fungu la maandiko.

1. Pale kama hakuna fungu la maandiko linalokubaliana na somo lako. Kama huwezi kupata fungu la maandiko lisilokubaliana na somo lako, kwanza jiulize, je, somo hilo ni la kibiblia au hapana?
2. Unaweza kupenda kushughulika na somo la Kibiblia lakini hakuna fungu la maandiko linalofanana na mawazo; kwa hiyo utapanua mawazo kupita upeo wa fungu moja.

C. Mapendekezo ya kawaida kuhusu namna ya kuchagua fungu la maandiko.

1. Fungu la kuhubiri lolote lisiwe ngumu la kueleweka.
   a. Wengine hawataona umuhimu wa kutunga hotuba kutokana na fungu kama hilo.
   b. Wengine hawatafahamu utakapokuwa umemaliza kwa sababu hawapendi kusikia vitu wanavyo vichukulia kuwa ni vya "kina," na kwa sababu ya muda mdogo huwezi kufafanua fungu kama hili.
   c. Wengine wanaweza kujisikia kwamba ulifanya hivyo kutokana na kupenda kuzungumzia "fungu ulilolipenda" au kuonyesha ufahamu ulio nao kuhusiana na vifungu wala sio kwa kusudi la kuwajenga.
   d. Kukitokea hitaji linalo hitaji kutumia fungu la maandiko ambalo ni gumu, basi tumia.
2. Unatakiwa kutumia sehemu zote za maandiko matakatifu, sio sehemu zile unazozipenda. Hubiri kutoka vitabu vyote 66
3. Jihadhari sana, usitumie maandiko matakatifu kutoka katika vifungu ambavyo watu wanavishuku.n Unaweza kuvitumia kama mfano sio kama fungu kuu la maandiko . (kwa mfano. 1Yohana 5:7, Yohana 7: 53-8:11)
4. Mahitaji ya wasikilizaji yanapaswa kufikiriwa unapochagua fungu la maandiko.
5. Kumbuka fungu la maandiko ulilolihubiri karibuni.
6. Matumizi ya fungu la maandiko ni kumaanisha kwamba, unafafanua fungu hilo la maandiko, unaelezea hoja yako. Ikiwa utalitumia tu mwanzoni mwa hotuba ya kitopiki na usilifafanue, wasikilizaji wengine watachanganyikiwa na kushindwa kuelewa.

## AINA YA HOTUBA

1. Ya kitopiko ( Somo)Topical

A. Kutokana na jina la hotuba hii, inashughulikia, topiki, somo, au kusudi.

1. Haiongozwi au kutawaliwa na fungu fulani.
2. Mifano ya hotuba kama hii: Imani, Maisha ya mkristo nk.(Lakini katika

masomo, itafahamika kwamba, inaweza kupunguzwa katika sehemu moja ili itumike katika wakati mmoja.

3. Nafuu ya hotuba za kitopiki(topical)
    a. Zinaweza kutumika wakati hitaji fulani linapojitokeza, lisiloweza kutatuliwa kwa kutumia hotuba zenye fungu kuu la maandiko(text).
    b. Kwa mfano somo kuhusu uovu wa dansi za siku hizi(kucheza).
    c. Inaweza kutumi pale somo linaloshughulikiwa linakamilishwa katika hotuba moja, linapaswa kuthibitishwa kutokana na vifungu kutoka sehemu mbali mbali za Biblia.
    d. Kwa mfano: Ni sala za aina gani anazozijibu Mungu? Zingatia kwamba hakuna msitari mmoja au fungu la maandiko moja litakaloweza kutoa mafundisho kuhusu sala.
4. Inaweza kufuatiwa na aina nyingi za utaratibu, kama ufafanuzi, habari kuhusu maisha

B. HATARI YA KUTUMIA HOTUBA ZA KITOPIKI(TOPICAL)
1. Inaweza ikawa ya namna moja(ya kufanana)
2. Inaweza isiwe kwa undani(maana yake ikawa haielezei maandiko kwa undani au kwa mapana.
3. Inaweza isiwe na utaratibu mzuri.
4. Inaweza isiwe ya kimaandiko kwa sababu vifungu vya maandiko ni rahisi kutolewa nje ya mazingira yake kwa kutaka kuunga mkono mawazo ya mhubiri.
5. ZINGATIA:Haya si matatizo yanayopatikana na kila hotuba ya kitopiki.

## II. YA KITEKSICHO( YENYE MSITARI MMOJA AU MIWILI)

A. Hii ni hotuba inayotumia maneno yale yale yanayopatika kutoka katika msitari mmoja au miwili kama pointi zake muhimu katika mwili zitakazo panuliwa mawazo yake jinsi mistari zitakavyofafanuliwa.
1. Maneno, mafungu, yatakayopatikana katika mistari, yatatumika kama pointi kuu zenyewe.
2 . Maneno yakiwa yamejiongeza, yakielezeka, katika maneno yanayofahamika, kwa wasikilizaji yanaweza yakatumika kama pointi kuu.

B. NAFUU YA HOTUBA YA KITEKSICHO(YENYE MSITARI MMOJA AU MIWILI)
1. Inamfanya mtoa ujumbe kuwa karibu na neno.
2. Ni rahisi kutengeneza.
3. Utangulizi hujengwa kwa kawaida kutoka ndani (mambo ya usuli, mazingira)
4. Wakati mwingine hatimisho hupatikana ndani ya fungu la maandiko.

C. HASARA YA UTARATIBU HUU.
1. Wasemaji wasio na mazoea wakati mwingine wanachagua fungu la maandiko lisilofaa kutumika kwa hotuba kama hizo.
2. Ni rahisi kujaribiwa kuuinua msitari au mistari kwa kuiondoa katika mazingira yake kwa sababu ya mgawanyiko uliyopo na kuzifanya pointi kuu.

## III. YA KUFUNUA WAZI (YA EKSIPOSITORE)

A. Hizi ni hotuba zinazochukuwa sehemu kubwa za maandiko matakatifu zenye wazo moja na kufunua yaliyomo au kuyaweka wazi kila sehemu yake kwa wasikilizaji katika njia ya kihotuba, ili pointi kuu zieleweke vizuri, na wasikilizaji kuona kwamba wamehusishwa.
1. Ni lazima iwe na zaidi ya mistari miwili. Sehemu ya fungu la maandiko linapaswa kuwa kubwa kiasi kwamba, pointi kuu zote zinapaswa kutoka ndani yake.
2. Inaweza kutokana na mistari michache, sura moja, kitabu kimoja au Biblia nzima.
3. Tofauti ya aina ya hotuba hii, na ile ya kiteksicho ni urefu wa maandiko matakatifu, maendeleo ya hotuba yatatokana na sehemu ya maandiko.

TAITO ( YENYE JINA)

1. KAZI YA YENYE JINA(TAITO)
   - A. Kuvutia na kuleta usikivu wa wasikilizaji wa somo.
   - B. Ni sawa na jina la kitabu- Haizungumzii kila kitu kuhusu hadithi, isipokuwa inakufanya upende kusoma.
   - C. Kazi yake kuu, ni kuweka katika matangazo gazetini.
2. TABIA AU NAMNA YA JINA.
   - A. Jina lisiahidi zaidi ya kile kitakachopatikana katika hotuba yenyewe.
   - B. Lisielezee kwa njia ya kukatisha tamaa.
   - C. Liwe la kusisimua(ili watu wasilidhalilishe wanapolisomo)
   - D. Liwe la kuvutia wasomoji.
   - E. Liwe rahisi, na lenye kukubalika katika jamii.
   - F. Hali yake inaweza kuwa kama ifuatayo:
     1. Ya namna ya swali
     2. Yenye mshangao
     3. Isio na sentensi nzima
     4. Isiwe yenye neno moja
     5. Isiwe ya mawazo yenye utata.
     6. Iwe chochote kinacholeta hamu kwa wasikilizaji.

KUJENGA HOTUBA

CHAGUA + ANDAA = UBUNIFU

I. KUKUSANYA MISTARI YAKUTUMIA KATIKA UJENZI WA HOTUBA.
   - A. AINA TATU YA YATAKIWAYO YA UBUNIFU WA INJILI.
     1. Maarifa
     2. Mawazo
     3. Mazoea ya mara kwa mara.

   - B. KINACHOWAFANYA WATOA HOTUBA KUISHIWA NA CHA KUWAHUTUBIA WATU.
     1. Pamoja na hitaji kubwa la mtoa hotuba kuwa mtu wa kiroho, mtoa hotuba anapaswa kuwa mbunifu.
   - C. MISTARI YA KUTUMIA IPATIKANE WAPI NA VIPI?

     1. Katika maandiko matakatifu:
        - a. Kwa kujifunza.
        - b. Fahamu kila fungu la maandiko, kila sura, sio kama kazi, au sio kwa sababu ya hotuba, au masomo ya darasani, au kama msaada katika hoja za kubishana, bali kama yale yanayohusu maisha yako.
     2. Kuwa na muda wa kimia wa kujifunza (1Pt. 2:2; Ebrania 5:14; Zaburi 119:9; Yohana 15:3; 17:17; 2Tim. 3:16, Efeso 6:17)
        - a. Yatakiwayo wakati wa kujifunza kimia:
          1. Mahali na muda maalum.
          2. Orodha ya sala
          3. Kajitabu kidogo ka kuwekea kumbukumbu
          4. Biblia
          5. Roho ya kutumaini.
        - b. Kanuni za muda wa kimia:
          1. Kusubiri. (haraka huua sala)
          2. Soma Biblia yako kwa sauti mara tatu.
          3. Tafakari yale unayoyasoma.
          4. Andika wazo kuu.
          5. Sali- Weka uwiano, imba sifa, omba.

6. Shirikisha – Waelezee wengine
7. Tii-Fanya. Kusulihisha bila matendo ni uongo…

3. SYSTEMATIC THEOLOGY(UTARATIBU UHUSIANAO NA THEOLOJIA)

   a. Kuwa na Itifaki ya Biblia (Kitabu cha orodha ya maneno ya Biblia)
   b. Fafanuzi za Biblia
   c. Kamusi za Biblia
   d. Esaklopedia (Vitabu vya elimu ya juu)

4. FILOSOFIA NA TABIA ZA WATU(Kufahamu mambo ambayo watu wamejaribu kutatua.) No.32
   ……………………………
5. SAYANSI(Kukusaidia kuwapata watu)
   a. Fisicholojia (Psychology) Kufahamu namna mtu anavyojimudu.)
   b. Sayansi ya asili (Kufahamu ulimwengu)
   c. Sosioloji na Athropoloji (Sociology and Athropology) Elimu ya kufahamu namna mwanadamu anavyoshirikiana na wengine.

6. Historia na maisha ya wahubiri na wazee wazamani.

7. Ukadiriaji wa hotuba yako.

MWILI WA HOTUBA YAKO

"Haitakiwi tu kutafuta mpango, bali uwe mpango mzuri."

I. MAELEZO: Mwili unakuwa na sehemu kubwa na ndogo ambazo zikikuzwa na kupangwa vizuri, zitatimiza kusudi la a wali lililomo katika **wazo kuu**.

II. KUSUDI NNE ZA KUWA NA MWILI WA HOTUBA.
   A. Kutoa habari- Kuelimisha kitu fulani, mfano, sifa za wazee.
   B. Kushawishi – Kufanya kuamini kitu fulani. Kwa mfano Biblia, na ugeuko.
   C. Kupata kutenda.- Fanya kitu fulani.
   D. Kuwatia moyo- Kujisikia. Kwa mfano furaha ya kumtumikia Mungu/ ukilinganisha na anasa za dhambi.
III. KAZI YA POINTI KUU
   A.. Kugawanya kimantiki wazo kuu katika sehemu.
   B. Kusaidia wazo kuu.
      1. Kufafanua wazo kuu.
      2. Kutia nguvu na kutaka vitendo kuhusiana na wazo kuu.

      3. Kuthibitisha wazo na maandiko matakatifu.
IV. MPANGO WA KUKUZA HOTUBA BORA UTATEGEMEA YAFUATAYO:
   A. Fanya mjio wako kuwa mpya na wakufahamika na wasikilizaji wako.
   B. Usitunge hotuba kwa kutumia utaratibu wa kidarasa.
   C. Baada ya kukuza mpango, shikilia hapo usiachilie.
   D. Hakikisha kila pointi yako ni ya kimaandiko na kuwa inaendelea vizuri.
   E. Tengeneza pointi zako na kuzizungumzia vizuri.(Usizisome tu pointi zako)
   F. Achana na maneno yasiotakikana.
   G. Tumia maneno yanayotakiwa sio kila neno.
   H. Kusanya mistari ya kutumia mingi kuliko ile utakayohitaji.]
      1. Mistari mingine unaweza kuzitumia kwa wakati ujao.

2. Mistari mingine itakusaidia kupanua maarifa.

I. Hakikisha autilaini utakayoitumia mimbarini imejaa vya kutosha kuwasilisha kila pointi vizuri.

J. Muda utakaoutumia katika pointi moja utaonyesha wasikilizaji wako umuhimu wa pointi yako.

K. Tawanya mistari ya kusisimua katika hotuba yako yote.

L. Husisha mwili na wazo lako kuu katika vitendo.

M. Tumia maneno ya wazi, mafupi, na meepesi yanayoeleweka.

N. Kushawishi kwa kutumia mistari , kuwa macho na mawazo ya wasikilizaji wako na kuwafurahisha ili waweze kuitikia mawazo yako.

O. ZINGATIA: Alama ya msemaji mzuri ni kuchukua kitu kigumu na kukifanya kuwa kiepesi.

V. MAPENDEKEZO KUHUSU POINTI KUU:

A. Zinapaswa kuwa na uzito au umuhimu unaofanana, na urefu sawa.

B. Mpangilio wake unapaswa kufanana.

C. Inapaswa kugawanya wazo kuu.

D. Ziwe ngapi?

1. Ya juu zaidi ni tano.
   a. Wasikilizaji wako hawawezi kushika zaidi ya pointi tano.
   b. Muda unaotolewa hauruhusu zaidi ya hiyo tano.
2. Ya chini sana ni mbili. Huwezi kugawanya kidogo ya hii.
3. Wazo kuu linapopangwa vizuri na kuchaguliwa vizuri, litatawala hesabu ya pointi zinazohitajika- Hakuna cha mazoea(mapokeo)
4. Kwa nini walio wengi wanatumia pointi tatu?
   a. Hazisumbui kukariri.
   b. Namba tatu ni ya kawaida katika maisha na Biblia. – Mwanzo, katikati, na mwisho. “Omba, tafuta, Bisha.

E. Zifanye ziwe rahisi za kukumbuka.

1. Rudia, rudia
2. Panga maneno kwa njia rahisi kukumbuka.
3. Msaada wa picha

F. Zipange ili ziweze kushika usikivu zitakapotajwa.(umuhimu wa vichwa)

G. Zielezee kufuatana na faida ya wasikilizaji (Linganisha na:-Paulo-“kwa “Mungu asiyejulikana” dhidi ya “kuumbwa kwa ulimwengu”

H. Zipange kwa kusudi la kuwavutia wasikilizaji wako wapate kuitikia.

I. Zinapaswa kuwa zenye mawazo yanayoendelea.

J. Pointi zinazoelezea kuhusu zingine zitangulie:

1. Za kupinga zitangulie za kukubaliana
2. Ya kimawazo itangulie ya kitu chenyewe.
3. Ya kawaida itangulie ya kawaida.
4. Mafundisho na ushawishi vitangulie ombi.
5. Makubaliano yatangulie kutokubaliana.
6. Ya rahisi itangulie ngumu.

K. Pointi kuu zote zinapaswa kutimiza W.K.

L. Kila pointi inapaswa kuelezewa wazi wazi, kwa kuzingatia, na kwa kukazia ili wasikilizaji wafahamu ni nini unachokizungumzia.

VI AINA YA POINTI KUU.

A. Mpangilio wa pointi zinazotumika katika vichwa vikuu.

1. Wakati uliopita, wakati wa uliopo, wakati ujao.
2. Kisababishi- Matokeo
3. Swali- Jibu.
4. Tia hatiani(dhambi), Shawishi (kuna mahali bora au kuna njia bora ya baraka)
5. Tatizo- Suluhisho
6. Nani, Nini, Kwa nini, Lini, wapi, jinsi gani,(munganiko wa aina yote) kwa mfano katika Wafilipi 4:13 – Nani?- mimi- Nini? Mambo yote- Jinsi gani? Katika yeye.

7. Fundisho- Ushikamanisho
8. Ya mwili, ya akili, ya kijamii, ya kiroho. (Luka 2:52)
9. Kanusha(vitu makosa)- Unga mkono(vitu vya kweli)
10. Mfanano- Utafauti (kwa mfano – Kanisa dhidi ya madhehebu)
11. Dalili,(kuzuia), ponya (mfano- uliburo au ulegezaji, kupenda dunia)
12. Hoja kuu na hoja ndogo, Hatimisho.

B. NAMNA YA MPANGILIO.

1. Picha ya mfano( Maisha ya askari dhidi ya maisha ya mkristo)
2. ABC au herufu zingine zikiwekwa pamoja.
3. Maneno yanayofanana.
4. Maneno ya kiakrostik
5. Kwa kutumia vitu vya asili( kujenga juu ya hatimisho ya kimantiki na kuomba)
6. Kuorodhesha(Kuorodhesha sababu)
7. Ya kufunua wazi (Eksipostore) (soma kazi ya watu kama G.Campbell Morgan, Spurgeon, McLaren, etc.)
8. Ya kimantiki.

VII. KUKUZA KWA POINTI NDOGO(Zile zote zinazosaidia pointi kuu)

A. Kusudi kuu- Kukuza pointi kuu ilizifahamike kimaandiko na kuwa na nguvu.

B. Pointi ndogo zinaweza kufanyika kutokana na kutumika kwa sababu zifuatazo:

1. Kuhusisha
2. Kuthibitisha (maandiko matakatifu NA ubishi- hakuna “Nafikiri”)
3. Namna wasikiliziji wanavyo jishughulisha katika hotuba.
4. Ufupisho(summaries)
5. wimbo
6. Shairi
7. Maelezo
8. Kwa kuainisha au kutofautisha (Ubatizo – Ebrania 6:2)
9. Maswali- Majibu
10. Pambanisho( Agano la kale dhidi ya Agano Jipia)
11. Mifano (hasa itoka katika Biblia)
12. Manukuu ( ukionyesha ni nani uliyemnukuu)
13. Mafundisho ya picha
14. Fafanusi
15. Usuli
16. Mantiki, ubishi, hoja

KUMKBUKA: USHAHIDI+HOJA= UTHIBITISHO

I. HATUA SABA ZA KUTAYARISHA HOTUBA

A. Sala

B. Mchangunuo wa wasikilizaji

1. Kwanza kulinga na mahitaji yao ya kiroho (wanao ijua na wanayoyajua)
2. Pili. Namna ya kuelezea kwa njia yenye mafanikio.

C. Amua wazo kuu.

1. Lipunguze ili litumike katika hotuba moja.
2. Chagua fungu la maandiko litakalo kwenda pamoja.

D. Andaa.

1. Amua pointi kuu zipi zitakazo kamilisha wazo kuu.
2. Kuza kila pointi kiasi cha kueleweka vizuri.
3. Hakikisha umeondoa mistari yote isiyohitajika

F. Rudia rudia kusomo hotuba yako ili ufahamu ni nini unachohitaji kuzungumzia.

G. Zoea kwa mdomo na kiakili.

1. Kujua ni nini unachotaka kusema
2. Kujua namna hasa unavyotaka kusema

II. CHIMBUKO LA MANENO UTAKAYOTUMIA

A. Kwa nini kunahitajika kutumia maneno yako mwenyewe?

1. Fikira huru husaidia kukuza, kutia nidhamu, na kutia uwezo wa kufikiri kwako.
2. Inafaidisha msemaji.
3. Inafanya wasikilizaji kuwa na matumaini katika msemaji.
4. Hasa mwaliko unapaswa kuwa wako mwenyewe.

B. Inawezekanaje kuwa yako mwenyewe?
1. Mawazo yako mwenyewe kuhusu maana ya maandiko.
2. Kuunganisha maandiko matakatifu na masomo pamoja na usikamanisho
3. Uchaguzi wa topiki(somo)
4. Ujenzi wa hotuba
5. Hali yako

C. Vizuizi vya kutumia yako mwenyewe:
1. Mawazo makosa
   a. Namna watu wanavyofikiri makosa kuhusu kuwa na yako mwenyewe.
      1. Je, yawe mapya kabisa? Hapana
      2. Tafsiri mpya
   b. Wengine wanadhani kwamba, kujifunza kwa mapana kunaingilia kuwa na maneno yako mwenyewe.

UTANGULIZI:

Kuanza vizuri ni nusu ya kumaliza lakini kuanza vibaya ni kuharibu kabisa.

I. SEHEMU YA UTANGULIZI:
   A. Kuteka usikivu, kuelezea wazo kuu, kuonyesha hitaji na kuorodhesha pointi.

II. KUSUDI LA UTANGULIZI:
   A. Kushika usikivu wa wasikilizaji.
   B. Kujifanyia nia nzuri kati yako na somo lako.
   C. Kuwaelekeza wasikilizaji wako katika somo.
   D. Kuwafanya wasikilizaji wako kusikiliza.

III. YANAYOTAKIWA NA YASIYOTAKIWA KUBORESHA UTANGULIZI
   A. Tumia sentensi fupi na yenye nguvu ikiwa na neno lako muhimu ndani yake.
   B. Kuwa anayevutia na anayependeza.
   C. Husisha utangulizi wako na somo.
   D. Tayarisha utangulizi wako vema.
   E. Jitenge na kuomba msamaha
   F. Anza kwa ujasiri na kwa shauku.
   G. Pata usikivu katika kipindi cha dakika kumi na usiupoteze.
   H. Subiri karibu sekunde mbili ili wasikilizaji wako wawe tayari.
   J. Waonyesha ni kwa nini wanapaswa kusikiliza.
   K. Wafahamu wasikilizaji wako ili kuwafikia iwe rahisi.
   L. Usiwe na mengi katika utangulizi, ingia upesi katika mwili wa somo lako.
   M. Hakikisha kwamba lina ubora wa kuteka usikivu wa wasikilizaji wako.
   N. Usije ukawachukulia wasikilizaji wako kuwa wanafahamu kile unacho wambia.
   O. Usitumie mifano isioendana na somo.
   P. Usiwafanye wasikilizaji wako kutarajia zaidi kutoka katika somo lako.
   Q. Neno lako la kuanza baada ya kusimama mbeli ya wasikilizaji wako, lisiwe, “somo letu leo”
   R. Usianze kwa kutazama chini.

IV. UTARATIBU UNAOTUMIK A KUANZA UTANGULIZI.
   A. Wimbo
   B. Sala
   C. Neno la mwanzo
   D. Neno tofauti linalogusia somo kwa umbali.
   E. Mifanyo mizuri/ Hadithi, mchezo)
   F. Habari kuhusu habari za mtu anayefahamika na wasikilizaji au na wewe.

G. Ingia katika somo mara moja.
H. Elezea lengo la somo lako
I. Elezea kusudi la kukutana kwenu.
J. Tumia vielelezo, Picha na kadhalika
K. Zaa hitaji la somo hilo ndani yao.
L. Onyesha haki yako kutoa hotuba hiyo
M. Elezea usuli wa somo lako ikihitajika.
N. Waondolee fikira makosa waliokuwa nazo.
Q. Wafanye wasikuone kama mjanja.
R. Waelezee matukio ya karibu wanayoyafahamu.
S. Elezea pointi kuu utakazo zungumzia.
T. Zungumza maana ya fungu lako la maandiko.
U. Kuwa tofauti na msemaji aliyetangulia.
V. Wasifu wasikilizaji wako.
W. Tumia fungu la maandiko, toa mazingira yake, usuli, sababu za kuchagua, na fafanusi kwa ufupi.

UKADIRIO

I. KUSUDI LA UKADIRIO:
   A. Kuonyesha udhaifu na nguvu zako.
   B. Kukusaidia ujione jinsi watu wanavyokuona.
      1. “Ukadirio wote ni sahihi”
      2. Bwana mmoja kwa jina la Somerset Maugham amesema, “Watu wanapenda ukadirio lakini wanapenda kupewa sifa tu.”

II. SEHEMU ZA UKADIRIO:
   A. SEHEMU KUU.
      1. Namna ya mpangilio wa hotuba.
         a. Kichwa(Jina)
         b. Fungu la maandiko kama lilihitajika
         c. Wazo kuu
         d. Utangulizi
      2. Yaliyomo katika hotuba.
      3. Sauti(Ilikuwa sauti ya kweli? Ilikuwa na mabadiliko mazuri?)
      4. Jumla ya jinzi hotuba ilivyotolewa.
   B. Sehemu za kukadiria kuhusu mtu binafsi.
      1. Alivyoonekana
      2. Nia aliyokuwa nayo kuhusu wasikilizaji wake.
      3. Sauti:
         a. Kiasi cha maneno. (Kwa dakika moja mtu anaweza kuzungumza maneno 125 lakini ubongo unaweza kufikiri maneno 1000 kwa dakika moja)
         b. Mbadiliko wa sauti(Kama ukadirio wa sauti kuwa ya juu au ya chini)
         c. Kukimia (sababu yetu kusema “uh” ni kwa sababu ya kusimama kusikohitajika.
         d. Mkazo(Kukazia katika kusema kwako, kutilia mkazo katika maneno fulani)
         e. Kiwango(kutoka juu hadi chini au toka chini hadi juu)
         f. Namna ya kuweka maneno yako( ukisimama kimantiki)
         g. Matamshi(kuyatamka maneno sahihi)
         h. Ufasaha(kusema maneno ili watu waweze kufahamu)
      4. Mpangilio:
         a. Mpangilio wa wazi
         b. Rahisi kwa watu wote kufuata hata pamoja na wewe.
         c. Je, ni kamilifu?
         d. Utangulizi

e. Mwili
f. Hatimisho
g. Kupisha( namna alivyohama kutoka pointi fulani kwenda nyingine)

5. Kupenda.
    a. Muda mrefu wa kusikiliza mazungumzo ni dakika 23
6. Umoja( wazo kuu)
7. Hitaji la wasikilizaji:
8. Mchanganuo wa wasikilizaji ulifanywa?
9. Je, alitimiza lengo lake?
10. Lugha:
    a. Je, alitumia lugha ya mitaani?
    b. Ulikuwa ndani sana( Kiyunani na Kiebrania)
    c. Gramma (------)
    d. Kuweka maneno(tunatakiwa kujitahidi kuyaweka maneno vizuri sio kusema tu)
11. Wiano.
    a. Je, anashika Biblia yake vizuri?
    b. Kusiwe na tabia ya kuondoa usikivu
    c. Unatakiwa kuonekana kuwa huru.
12. Kutazama wasikilizaji( unatakiwa kuwatazama wasikilizaji wako daima)
13. Shauku.
    a. Katika sauti yako na mwili wako pia.
        1. Katika sauti(kubadilika kwa sauti)
        2. Kimwili(Unahitaji kuwa na uhai)
14. Kuhusisha wasikilizaji.
    a. Katika kila hotuba huwahubiri watu wengine mahali pengine, bali ni hao watu sasa.
15. Je, maelezo yalikuwa katika upendo?
16. Je, ilishikilia kupenda.
17. Mifano.
    a. Hotuba ilikuwa na mifano ya kutosha?.(angalia hotuba za Yesu)
    b. Je, kulikuwa na mifano ya kutosha?
    c. Je, ilihusu watu binafsi?
    d. Je, ilikuwa ya kufurahisaha?
18. Matumizi ya maandiko matakatifu.
    a. Je, kulikuwa na maandiko ya kutosha?
    b. Je, yalikuwa mengi kuzidi?
    c. Je, yalifafanuliwa?
    d. Je, yalisoma wazi wazi na vizuri?
    e. Je, yalitumiwa vizuri?
19. Maandalizi.

III. NAMNA YA KUTOA UKADIRIO.
- A. Kuwa mwaminifu na wakulenga
- B. Daima toa mapendekezo ya kuboresha.
- C. Kazia tu makosa makubwa makubwa.

IV. NAMNA YA KUPOKEA MAKADIRIO
- A. Tunza makadirio na kuyaangalia ili kuboresha.
- B. Uliza maswali lakini usijaribu kujitetea katika kila pointi.
- C. Usifikirie makosa yako yaliyopita unapotoa hotuba.
- D. Usikate tamaa, bali yapokee kama changamoto.
- E. Njia sita za kutenda (kujibu mashambulizi)
    1. Nenda nyumbani na kulia.
    2. Chukia.
    3. Jisikitikie.

4. Pofuka na kutokujiona, na kutoa udhuru. Mtu asiye pokea ukadirio kwa furaha darasani, hatapokea akiwa kazini.
5. Tumia ukadirio kuboresha- “sio lazima uwe mkamilifu wewe mwenyewe ndipo utoe ukadirio vizuri .

## KUPISHA (UPISHANO)

UTANGULIZI:

A. Mazungumzo mazuri ni munganiko wa vipengele mbali mbali viliowekwa kwa pamoja katika viungo pishano.

B. Ulinganisho kati ya upishano na daraja.

I. KAZI YAKE:

A. Kuwezesha hotuba kutiririka kwa ulaini.

B. Inaonyesha wasikilizaji

# ARUSHA BIBLE SCHOOL

MUHULA WA TATU
MWAKA WA KWANZA 2001
HOMELETIKSI

MTIHANI WA MWISHO

JINA LA MWANAFUNZI__________________________TAREHE 04/10/2001

1. Kati ya kusudi tatu za kozi hii, elezea moja. ____________________________
   ________________________________________________________________

2. Homiletiksi maana yake ni nini?______________________________________

3. Kuelezea watu ukweli wa dini unaopatikana katika maandiko matakatifu, wenye kushawishi huitwa nini?_________________________

4. Hotuba inaonekana imefaulu mambo matano yakiwa yametendeka, taja mawili kati ya hayo matano:

**ARUSHA BIBLE SCHOOL**

MUHULA WA TATU
MWAKA WA KWANZA 2001
HOMELETIKSI

MTIHANI WA MWISHO

JINA LA MWANAFUNZI_________________________TAREHE 04/10/2001

1. Kati ya kusudi tatu za kozi hii, elezea moja. ___________________________
   ____________________________________________________________

2. Homiletiksi maana yake ni nini?___________________________________

3. Kuelezea watu ukweli wa dini unaopatikana katika maandiko matakatifu, wenye kushawishi huitwa nini?_______________________

4. Hotuba inaonekana imefaulu mambo matano yakiwa yametendeka, taja mawili kati ya hayo matano:

   1.____________________________________________________________

   2.____________________________________________________________

5. Kuna mahitaji kadhaa kwa mahubiri au mafundisho yenye mafanikio

   A. Kuwa mtu wa kiroho,vipawa vya asili,maarifa, ujuzi
   B. Kuwa mtu mpole, Kuwa mtu wa kiroho, maarifa, ujuzi
   C. Kujazwa na Roho, Kusaidia, kufundisha. Kuimba.

6. Katika malengo ya kozi hii, kuna mambo manne, taja moja.

   a.______________________________________________

7. Kuhusu hofu ya jukwani, kuna visabibishaji vitatu, taja kimoja:
   A_________________________________________________

8. Kuna dalili 13 za hofu ya jukwani taja mbili:
   a.___________________________b.____________________________

9. Kuna aina 11 ya msaada katika kuondoa hofu ya jukwani, taja 2
   a.___________________________b._____________________________

10. Kuna thamani ya hofu ya jukwani tatu taja moja.

    a._________________________________________________________

11. Kusudi na maana ya mchanganuo ni nini?
    A.Inaamua ni nini utakacho wafundisha watu, Inaamua mjio gani utakaoutumia
    B.Inaamua ni muda gani utaanza kufundisha, Inaamua imani ya watu
    C.Inaamua ni nini utakacho wafundisha watu, Inaamua ni muda gani utaanza Kufundisha

12. Namna ya kuandaa somo lako kufuatana na hali nne ya wasikilizaji wako
    A.Mapokezi ya kirafiki, yakutojali-kuwapo lakani anajali kidogo, wenye

Wasiwasi, wanaogopa.
B.Ya kutojua ukweli, yakutojali kuwapo lakini anajali kidogo, wenye wasiwasi
C.Mapokezi ya kirafiki, yakutojua ukweli,wenye wasiwasi, wanaogopa.|

13. Kuna maneno sita yenye maana ileile na neno WAZO KUU. Taja mawili kati ya hayo: (1)____________________(2)_____________________

14. Katika kila hotuba ni lazima kuwa na wazo kuu ngapi lenye kuongoza utaratibu mzima na kusudi la somo? ___________________________________

15. W.K. maana yake ni nini?______________________

16. Ni nini umuhimu wa wazo kuu?

A.Kuhakikisha umoja katika hotuba, kuondoa mambo ambayo hayafai katika ujumbe.
B.Kuonyesha ujuzi wa mtoa hotuba, kuondoa wasiwasi kwa wasikilizaji wako
C.Kuboresha hotuba yako, Kufanya mahubiri yako kuwa yakuvutia.

17. Kuna mapendekezo 9 kuhusu insha(w.k.) taja mbili kati ya hizo 9:
a.___________________________________________________

b.____________________________________________________

18. Namna ya kuchagua na kuamua W.K. yako inahitaji mambo 5 taja moja kati ya hayo 5. (1)______________________________________________________

19. Ubora wa hotuba utategemea ubora wa nini?

A.Wa mhubiri mwenyewe B. Autilaini C. Wasikilizaji

20. Sehemu kuu 3 za hotuba katika autilaini ni zipi?

A.Utangulizi , Wazo kuu, Hatimisho

B.Utangulizi , Mwili, Hatimisho

C.Utangulizi,Hatimisho, Hoja

21. Hotuba zima ni kama duara ama tairi la baiskeli:
1.Wazo kuu ni kama nini?____________________________________
2.Spoke za baiskeli ni kama nini katika hotuba?___________________

22. Kuna mapendekezo kuhusu hatimisho 20 taja tatu kati ya hizo 20

a.__________________________________________________________

b.__________________________________________________________

c.___________________________________________________________